



UPATIKANAJI Mapema

Kwa ajili ya watoto wachanga, watoto wanaoanza kutembea na familia

## Sehemu C ya IDEA

# Mwongozo wa Utaratibu wa Ulinzi kwa Wazazi (Haki za Mzazi katika Kuingilia Kati Mapema)

Septemba 2019

Idara ya Elimu Iowa, Wakala Kiongozi  
Taasisi ya Mikakati na Misaada ya Wanafunzi  
Grimes State Office Building  
Des Moines, IA 50319

**Jimbo la Iowa Idara ya  
Elimu**

Grimes State Office Building  
400 E. 14<sup>th</sup> Street  
Des Moines, IA 50319-0146

**Bodi ya Elimu ya Jimbo**

Rosie Hussey, Rais, Clear Lake  
Charles C. Edwards, Jr., Makamu wa Rais, Des Moines  
Diane Crookham-Johnson, Oskaloosa  
Sister Jude Fitzpatrick, West Des Moines  
Michael L. Knedler, Council Bluffs  
Valorie J. Kruse, Sioux City  
Mike May, Spirit Lake  
Max Phillips, Woodward  
LaMetta Wynn, Clinton  
Edgar Thornton, Mjumbe Mwanafunzi, Mji la Iowa

**Utawala**

Brad A. Buck, Mkurugenzi na Afisa Mtendaji wa Bodi ya Elimu ya Jimbo

**Kitengo cha Mafunzo na Matokeo**  
W. David Tilly, Naibu Mkurugenzi  
Mary Delagardelle, Mtawala Mshiriki wa Kitengo  
Thomas A. Mayes, Wakili

**Taasisi ya Mikakati na Misaada ya wanafunzi**

Sarah Brown, Mkuu  
LauraBelle Sherman-Proehl, Mshauri wa Kiutawala  
Cindy Weigel, Mshauri

Ni sera ya Idara ya Elimu ya Iowa kutobagua kwa kigezo cha mbari, imani, rangi, ujinsia, jinsia, taifa asili, jinsi, ulemavu, dini, umri, chama cha siasa, au hadhi halisi au kisi ya mzazi, familia au ndoa katika mipango yake, shughuli zake au ajira kaka inavyohitajika na Kanuni za loa vifungu 216.9 and 256.10(2), Vichwa VI na VII vya Sheria ya Haki za Raia ya 1964 (42U.S.C. § 2000d na 2000e), Sheria ya Malipo Sawa ya 1973 (29 U.S.C. § 206, et seq.), Kichwa IX (Marekebisho ya Elimu,, 20 U.S.C. §§ 1681 – 1688), Kifungu 504 (Sheria ya Matibabu ya 1973, 29 U.S.C. § 794), na Sheria ya Idara ya Elimu kwa Watu wenye Ulemavu (42 U.S.C. § 12101, et seq.). Kama una maswali au malalamiko kuhudu kukubaliana na sera hii kwa Idara ya Elimu ya Iowa, tafadhalii wasiliana na mshauri wa sheria kwa ajili ya idara ya Elimu Iowa, Grimes State Office Building, 400 E. 14<sup>th</sup> Street, Des Moines, IA 50319-0146, simu namba: 515-281-5295, au Mkurugenzi wa Ofisi ya Haki za Raia, U.S. Idara ya Elimu, Citigroup Center, 500 W. Madison Street, Suite 1475, Chicago, IL 60661-4544, namba ya simu: 312-730-1560, namba ya FAKSI: 312-730-1576, namba ya TDD: 877-521-2172, barua pepe: [OCR.Chicago@ed.gov](mailto:OCR.Chicago@ed.gov).

## **YALIYOMO**

Utagulizi .....	1
Maana Muhimu.....	2
Idhini Iliyotaarifiwa.....	3
Walaka wa Maandishi wa kabla.....	4
Usiri wa Taarifa / Kumbukumbu.....	5
Mikutano.....	9
Wazazi na wazazi mbadala.....	10
Chaguzi za Utatuzi wa Migogoro.....	12
Upatanisho.....	13
Malalamiko ya Jimbo ya IDEA .....	15
Malamiko ya Taratibu za Malipo (Kusikilizwa kesi za Taratibu za Malipo).....	17
Nakala ya Fomu: Ombi la Mkutano wa Usuluhishi.....	20
Nakala ya Fomu: Malalamiko ya Jimbo ya IDEA.....	22
Nakala ya Fomu: Malalamiko ya Taratibu za Malipo (Ombi la Kesi ya Utaratibu wa Malipo) .....	24
Sera za Mfumo wa Malipo.....	26

## UTANGULIZI

UPATIKANAJI Mapema ni ushirikiano kati ya familia na watoto wao wadogo wenye mahitaji maalumu (kuanzia kuzaliwa hadi miaka mitatu) na watoa huduma kutoka Idara ya Elimu, Afya ya Umma, na Huduma za Kibinadamu za Iowa na Kliniki za Wataalamu wa Afya ya Mtoto katika Chuo Kikuu cha Iowa. Dhumuni la ushirikiano huu ni kufanya kazi pamoja katika kuainisha, kuratibu na kutoa huduma za kuingilia zinazohitajika mapema na rasilimali ambazo zitasaidia familia kuwasaidia watoto wao wachanga au watoto wanaoanza kutembea kukua na kuendelea.

Wazazi wana haki, zinazojulikana kama utaratibu wa ulinzi, ambao unatumika katika kila nyanja za hatua za kuingilia kati mapema, kama vile tathmini, upatikanaji wa kumbukumbu, na timu ya Ushiriki Mpango wa Huduma za Familia Binafsi (IFSP). Sheria na taratibu za Jimbo na shirkisho zinaonyesha kinachotakiwa kutokea kwa watoto wachanga na wastahilifu na watoto wanaoanza kutembea wenye hali au wanaochelewa kukua na kuendelea.

Nyaraka hii inafanyakazi kama wakala **wako** wa utaratu wa ulinzi na utakusaidia kuelewa haki ulizonazo wewe na kwa mtoto wako kupitia sheria ya shirkisho, *Sheria ya Elimu kwa watu wenye Ulemavu (IDEA) Sehemu C*, vile vile *Sheria za Kiutawala kwa ajili ya UPATIKANAJI Mapema kuhusisha Mfumo wa Huduma za Kuingilia kati Mapema wa Iowa*.

kwa taarifa zaidi kuhusu haki yako, wasiliana na yeyote kati ya

wafuatao: Mratibu wako wa Huduma

Mdhamini wako wa Mkoa (Ulizia Mkurugenzi wa Elimu Maalumu)

Idara ya Elimu Iowa

Taasisi ya Mikakati na Misaada ya Wanafunzi

Grimes State Office Building

Des Moines, Iowa 50319-0146

515-281-3176

Kituo cha Rasilimali ASK, Kituo cha Mafunzo na Taarifa cha Wazazi Iowa

5665 Greendale Road, Suite D

Johnston, IA 50131

1-800-450-8667

515-243-1713

FAX 515-243-1902

[info@askresource.org](mailto:info@askresource.org)

<http://www.askresource.org>

Haki za Watu Wenye Ulemavu Iowa

400 East Court Avenue Suite 300

Des Moines, Iowa 50309

515-278-2502

515-278-0571 (TDD)

800-779-2502

515-278-0539 FAX

[info@disabilityrightsowa.org](mailto:info@disabilityrightsowa.org)

<http://www.disabilityrightsowa.org>

## **Lini nitapata nakala ya Utaratibu wa ulinzi/Haki za familia?**

Utapata nakala ya utaratibu za ulinzi/haki za familia angalau mara moja kila mwaka, na wakati wowote unapoiomba. Utapatiwa pia nakala hiyo kila upatapo walaka wa maandishi kabla. Fomu ya wakala wa maandishi wa kabla itajumuisha anuani ya mtandao kwaajili ya utaratibu wa ulinzi.

## **Kuna vyanzo vyovoyote vya taarifa ili kujua zaidi kuhusu IDEA 2004 Sehemu C, Sheria za Kiutawala za Iowu kwa ajili ya UPATIKANAJI Mapema, na sheria na taratibu zingine ambazo ni muhimu kwangu kuzifahamu?**

Zifuatazo ni anuani za toviti ambazo unaweza kutembelea:

Sheria za Kiutawala za Iowu kwa ajili ya UPATIKANAJI mapema

<http://www.educateiowa.gov>

Sheria ya Elimu wa watu Wenye Ulemavu

<http://idea.ed.gov/part-c/search/new>

Sheria ya Haki za Kielimu na Faragha kwa Familia (FERPA)

<http://www.ed.gov/policy/gen/guid/fpcbo/ferpa/index.html>

Sheria ya Uwezekano na Uwajibikaji wa Bima ya Afya (HIPAA)

<http://www.hhs.gov/ocr/hipaa/>

Wasilaiana na mratibu wako wa huduma kwa ajili ya rasilimali zingine. Unaweza kujerea kwenye:

*Urekebishaji wa mambo Yanapokwenda Vibaya*

*Rahisi! Urekebishaji mambo na Mwezeshaji wa Utatuzi*

*Kuijandaa kwa ajili ya Kurejea Tena au Upatanisho*

*Upatanisho kuhusu Elimu Maalumu: Mwongozo kwa ajili ya Wazazi*

## **MAANA MUHIMU**

**Wakala wa Umma:** Wakala Kiongozi (Idara ya Elimu Iowu) na vijisehemu vingine vya kisiasa vya Jimbo ambavyo vinawajibika kwaajili ya utaoaji wa huduma za kuingilia kati mapema kwa watoto wanaostahili chini ya IDEA na sheria za UPATIKANAJI mapema. Idara ya Elimu Iowu inawajibika kwa ajili ya malalamiko ya UPATIKAJANI mapema/ mfumo wa taratibu za malipo.

**Mdhamini/Mdhamini wa Mkoa:** mpokeaji wa fesha za shirikikisho Sehemu C au fedha za Taifa ambaye ana wajibu kisheria na kiuchumi katika kuhakikisha mfumo wa UPATIKANAJI mapema unafanyiwa kazi kimkao.

**Huduma za Kuingilia Kati Mapema:** huduma za kimaendeleo ambazo zinatolewa chini ya usimamizi wa umma; zinatolewa bila malipo isipokuwa pale ambapo Shirikisho au Sheria ya Jimbo inatoa kwa ajili ya mfumo wa malipo; na zimebuniwa kutimiza mahitaji ya kimaendeleo ya mtoto mchanga na mtoto anayeanza kutembea mwenye ulemavu, kama ilivyobainishwa na timu ya Mpango wa Huduma ya Familia Binafsi.

Huduma ziko katika moja ua zaidi ya maeneo ya kimaendeleo yafuatayo: maendeleo ya kimwili, kitambuzi, mawasiliano, kijamii/kihisia, au maendeleo yanayobadilika.

**Mtoto mchanga au Mtoto anayeanza Kutembea mwenye Ulemavu:** mtu mwenye umri chini ya miaka 3 ambaye anahitaji huduma za kuingilia kati mapema kutokana na kuchelewa kuendelea, kama ilivyopimwa na kifaa sahihi cha uchunguzi na taratibu katika eneo 1 au zaidi ya maendeleo ikiwemo kitambuzi, kimwili, mawasiliano, jamii/hisia, na yanayobadilika; au kwasababu ya hali ya kimwili au kiakili iliyozunguzwa ambayo ina uwezekano mkubwa wa kupelekea kuchelewa kuendelea.

## IDHINI ILIYOTAARIFIWA

### **“Idhini” ina maana gani?**

Idhini kutokea pale ambapo mahitaji yote matatu ya fuatayo yamefikiwa:

1. Ume Fahamishwa kikamilifu taarifa zote zinazohusiana (“muhimu”) na shughuli ambayo idhini yako inahitajika, katika lugha yako ya asili.
2. Una elewa na kukubali, kimaandishi, shughuli ambayo idhini inahitajika. (fomu ya idhini lazima ielezee shughuli na iorodheshe kumbukumbu za kuingilia kati mapema (kama zipo) ambayo itatolewa na itatolewa kwa nani.)
3. Una elewa kwamba kutoa idhini ni hiari na unaweza kusitisha idhini yako wakati wowote.

### **Wakati gani idhini ya wazazi iliyotaarifiwa inahitajika?**

Idhini yako inahitajika kabla:

1. Mdhamsini wa Mkoa au wakala wa UPATIKANAJI Mapema hajampa mtoto wako utaratibu wa hiari wa uchunguzi wa afya kubaini iwapo wakala anahisi mtoto wako anaweza kuwa na ulemavu;
2. Tathmini na chunguzi zote za mtoto wako na familia yako;
3. Mtoto na familia yako kupokea huduma za UPATIKANAJI Mapema;
4. Kutumia bima ya umma au binafsi kujumuisha mtoto wako au familia yako (angalia ukurasa wa 26 hadi 35), isipokuwa idhini yako haihitajiki; na
5. Kuweka wazi taarifa binafsi zinazotambulika kutoka kwenye kumbukumbu za mtoto wako za UPATIKANAJI Mapema, isipokuwa idhini yako haihitajiki.

Iwapo ukikataa kutoa idhini yako chini ya kipengele 1, 2, au 3, Mdhamsini wa Mkoa au wakala mwingine wa UPATIKANAJI Mapema lazima achukue hatua stahiki kuhakikisha kwamba (a) unafahamu kikamilifu asili ya tathmini, uchunguzi, au huduma ambazo zinaweza kuwepo kwa ajili ya mtoto wako, na (b) una elewa kwamba mtoto wako hataweza kupokea tathimini, uchunguzi au huduma hadi utoe idhini.

Iwapo utatoa idhini yako kwa huduma za UPATIKANAJI Mapema, lazima ianze haraka iwezekanavyo baada ya wewe kutoa idhini.

### **Nini kitatokea kama nifuta idhini yangu kwaajili ya huduma?**

Idhini yako ni ya hiari na inaweza kufutwa wakati wowote; hata hivyo, haiathiri kitendo kilichofanyika baada ya idhini kutolewa na kabla ya idhini kufutwa. Unaweza kukataa au kufuta idhini yako kwa huduma maalumu ya kuingilia kati mapema bila kuhtarisha huduma zingine za UPATIKANAJI Mapema kwa mtoto wako.

**Iwapo nikikataa idhini yangu, Mdhamsini wa Mkoa au wakala mwingine wa UPATIKANAJI Mapema ataweza kutumia taratibu za Malipo za IDEA kutia changamoto kukataa kwangu kutoa idhini?**

Hapana.

**Iwapo nikikatisha idhini yangu, naweza kumfanya Mdhamsini wa Mkoa kuharibu kumbukumbu za mtoto wangu za UPATIKANAJI Mapema?**

Hapana.

## **WALAKA WA MAANDISHI WA AWALI**

Ushiriki wako katika maamuzi kwa ajili ya maendeleo ya mtoto wako ni muhumu. Sheria zinahitaji kwamba unahusika wakati wa shughuli maalumu zinazoambatana kwakuwa hizi zinaathiri huduma za kuingilia kati mapema za mtoto wako.

“Walaka wa Maandishi wa Kabla” ni mawasiliano ya maandishi kwako kutoka kwa mratibu wa huduma wakati mto huduma anapendekeza au anakataa kuanzisha au kubadili ubainishaji, tathmini au hali ya mtoto wako au utoaji wa huduma sahihi ya UPATIKANAJI mapema kwa mtoto wako na/au familia.

Walaka huo lazima upewe ndani ya muda unaostahiki baada ya maamuzi ya mtoaji huduma juu ya pendelezo au kukataliwa kufanya lakini *kabla* ya mto huduma hajatekeleza hatua hiyo.

### **Taarifa gani inajumuishwa kwenye walaka?**

Walaka lazima uwe na yafuatayo:

1. Maelezo ya hatua iliyopendekezwa au kukataliwa;
2. Maelezo ya kwanini hatua imependekezwa au imekataliwa;
3. Utaratibu wa ulinzi uliopo; na
4. Namna ya kufungua malalamiko ya Jimbo au malalamiko ya hatua za malipo (na muda) ambao unaamini mahitaji ya UPATIKANAJI wa Mapema yamekiukwa.

### **Walaka unafananaje?**

Itakuwa fomu, ilioandikwa kwa lugha ambayo inaeleweka na umma. Itakuwa katika lugha yako ya asili. Kama lugha yako ya asili (au njia nyingine ya mawasiliano) si lugha ilioandikwa, mto huduma atachukua hatua ya kuhakikisha kwamba unauelewa walaka huo. Kama wewe ni kiziwi au kipofu, au huna lugha ilioandikwa, mawasiliano yatakuwa yale ambayo kwa kawaida unayatumia (kama vle lugha za alama, nukta nundu au mawasiliano ya mdomo).

### **Itakuwaje kama sikubaliani na hatua iliyopendekezwa au kukataliwa?**

Kuna chaguzi nyingi rasmi na zisizo rasmi zinazopatikana kwaajili yako. Zimeelezewa kwenye sehemu ya “Chaguzi kwa ajili ya Utatuvi wa Migogoro” katika kijitabu hiki. Mratibu wako wa huduma yupo kukusaidia kuelewa uchaguzi wako. Nyenzo zingine zimeorodheshwa kwenye sehemu ya utangulizi iliyopo mbele ya mwongozo huu.

Kwa maombi, mratibu wako au wakala wa umma atakujulisha juu ya huduma zozote za kisheria za bure au za malipo ya chini na huduma zingine za msaada katika eneo lako.

### **MAELEZO:**

## **USIRI WA TAARIFA/KUMBUKUMBU**

IDEA na sheria nyingine ya shirikisho inayoitwa Haki za Elimu ya Familia na Sheria ya Faragha (FERPA) zinakupa haki kadhaa kuhusu kumbukumbu za UPATIKANAJI Mapema za mtoto wako. Una haki ya kupata hizo kumbukumbu na una haki ya kuhoji mambo ambayo unadhanani hayako sahihi katika hizo kumbukumbu. Taarifa binafsi kwenye kumbukumbu za UPATIKANAJI Mapema za mtoto wako ni siri, na lazima zisitolewe bila idhini yako (isipokuwa kitu kisichokuwa cha kawaida kwenye idhini kinatumika). Kifungu hiki kinatoa taarifa zaidi kuhusu kinga hizo muhimu.

### **Naweza kupata kumbukumbu za mtoto wangu za UPATIKANAJI Mapema?**

Ndiyo. Wakala wa umma lazima ukuruhusu kukagua na kuitia kumbukumbu za mtoto wako za kuingilia kati mapema kuhusiana na tathmini na uchunguzi, utambuzi wa ustahilifu, maendeleo na utekelezaji wa IFSP, malalamiko binafsi kuhusu mtoto wako, na eneo lingine linalohusisha kumbukumbu kuhusu mtoto na familia yako. Wakala wa umma lazima, kwa maombi yako, akupe orodha ya aina na mahali kumbukumbu za UPATIKANAJI Mapema zinakusanywa, zinatunzwa, au zinatumwi na wakala.

### **Lini wakala wa umma atanipa kumbukumbu za mtoto wangu za UPATIKANAJI Mapema?**

Wakala wa umma atakubali ombi la kuitia au kukagua kumbukumbu bila kuchelewa kusiko kwa lazima – si zaidi ya siku 45 baada ya kuombwa na kabla ya mukutano wowote kuhusiana na IFSP au shauri lolote.

### **“Haki ya kukagua na kuitia” inajumuisha nini?**

Haki ya kukagua na kuitia inajumuisha yafuatayo:

1. jibu kutoka kwa wakala anayehusika na maombi ya kweli kwa ajili ya maeleo na tafsiri ya kumbukumbu;
2. ombi la kumtaka wakala atoe nakala za kumbukumbu zenyе taarifa (akishindwa kutoa nakala hizo atakuzuia kutekeleza haki yako ya kukagua na kuitia kumbukumbu); na
3. kuwa na mwakilishi wa kukagua na kuitia kumbukumbu.

Wakala anafikiri kwamba una mamlaka ya kukagua na kuitia kumbukumbu za mtoto wako isipokuwa wakala ameshauriwa kwamba huna mamlaka chini ya sheria ya Serikali inayoongoza masuala hayo kama mlezi, kutengena au talaka.

### **Wakala ataweka kumbukumbu ya mtu aliyeangalia kumbukumbu za mtoto wangu za Kuingilia kati Mapema? Ndiyo. Isipokuwa zionyeshwe kwa wazazi na mfanyakazi wa wakala aliyeidhinishwa, wakala anayetunza kumbukumbu ataweka kumbukumbu za pande zote zilizopata kumbukumbu za kuingilia kati mapema, ikiwemo:**

1. Jina la pande husika;
2. Tarehe upatikanaji ulipotolewa; na
3. Dhumuni ambalo pande husika inaruhusiwa kutumia hizo kumbukumbu.

### **Nini kitatokea iwapo kumbukumbu zina taarifa za mtoto zaidi ya mmoja?**

Una haki ya kukagua na kuitia taarifa zile tu zinazohusiana na mtoto wako au kujulishwa hizo taarifa mahususi.

## **Wakala anaweza kunitoza malipo ya kukagua na kupertia kumbukumbu za mtoto wangu za UPATIKANAJI Mapema?**

Wakala anayeshiriki anaweza kukutoza malipo kwa ajili ya nakala za kumbukumbu ambazo ulizotengenezewa kama malipo hayo hayakuzuii wewe kutekeleza haki yako ya kukagua na kupertia hizo kumbukumbu. Wakala hawesi kukutoza malipo kwa ajili ya kutafuta au kurekebisha taarifa hizo.

## **Kuna kumbukumbu ambazo lazima upewe bure?**

Ndiyo. Wakala wa UPATIKANAJI Mapema lazima akupe nakala ya kila tathmini, uchunguzi wa mtoto, uchunguzi wa familia, au Mpango wa Huduma za Familia Binafsi (IFSP) haraka iwezekanavyo baada ya kila mukutano wa IFSP.

## **Nini kitatokea kama kinihisi kwamba taarifa zilizoko kwenye kumbukumbu si sahihi?**

Kama unaamini kwamba taarifa zilizokusanywa, kutunzwa au kutumika si sahihi, zinapotosha au zinakiuka faragha au haki zingine za mtoto wako unaweza kumwomba wakala anayetunza kumbukumbu kuzirekebisha. Wakala ataamua ndani ya muda unaofaa iwapo taarifa irekebishwe kwa kulingana na ombi husika. Iwapo wakala anaamua kukataa kurekebisha taarifa hiyo kulinga na na ombi husika, atakujulisha juu ya kukataa na kukushauri juu ya haki ya kusikilizwa.

Kwa maombi yako, wakala atatoa fursa kwa ajili ya kesi kuhoji taarifa iliyoko kwenye kumbukumbu za kuingilia kati mapema kuhakikisha kwamba si sahihi, inapotosha au pengine inakiuka faragha au haki zingine za mtoto wako. Kama matokeo ya kesi:

1. Iwapo maamuzi ni kwamba taarifa imepotoshwa, si sahihi au pengine inakiuka faragha au haki zingine za mtoto, wakala atarekebisha taarifa inavyotakiwa na kukujulisha kwa maandishi.
2. Iwapo maamuzi ni kwamba taarifa **si** sahihi, imepotoshwa au pengine inakiuka faragha au haki zingine za mtoto, wakala atakujulisha juu ya maamuzi. Wakala pia atakujulisha haki yako ya kuweka kwenye kumbukumbu inayotunzwa kuhusu mtoto wako maelezo juu ya taarifa na kutoa sababu za kutokubaliana na maamuzi ya wakala.
3. Maelezo yoyote yaliyowekwa kwenye kumbukumbu za mtoto wako lazima zitunzwe na wakala kama sehemu ya kumbukumbu ilimradi kumbukumbu au sehemu yenye mgogoro inatunzwa na wakala. Iwapo kumbukumbu au sehemu yenye mgogoro ya kumbukumbu imewekwa wazi kwa upande wowote na wakala, maelezo yako lazima pia yawekwe wazi.

## **Kesi itafananaje?**

Kesi lazima ikubaliane na mahitaji ya FERPA. Mahitaji hayo yanapatikana kwenye 34 C.F.R. Kifungu 99.22. Wasiliana na mratibu wako wa huduma kama iwapo ungetaka taarifa kuhusu mahitaji hayo.

### **“Taarifa binafsi za utambuzi” inamaana gani?**

Utambuzi binafsi unamaana kwamba taarifa zinajumuisha, lakini si ukomo:

- Jina la mtoto wako
- Jina lako au majina ya wanafamilia yako
- Anuani ya mtoto wako au yako au wanafamilia
- Kitambulisho cha mtoto wako, kama vile namba ya hifadhi ya jamii ya mtoto wako, namba ya mwanafunzi au kumbukumbu za kibaometriki
- Vitambulisho vingine vsisivyo vya moja kwa moja, kama vile tarehe ya kuzaliwa ya mtoto, mahali alipozaliwa au jina la mama
- Taarifa zingine ambazo pekee au pamoja zimeunganishwa au zinaunganishwa kwa mtoto husika ambazo zitawezesha mtu husika kwenye jamii, ambaye hana ufahamu juu ya matatizo, kumtambua mtoto kwa ujasiri.
- Taarifa zilizoombwa na mtu ambaye wakala anaamini anafahamu kitambulisho cha mtoto ambaye kumbukumbu zinaendana naye.

### **Wakala ambaye ana kumbukumbu za mtoto wangu za UPATIKANAJI Mapema anahitajika kuniomba ruhusa kuachilia taarifa?**

Ndiyo, kama sheria kuu. Idhini ya mzazi lazima ipatikane kabla ya taarifa za utambulisho binafsi kutolewa kwa mtu yeyote (zaidi ya maofisa, wawakilishi wenye kibali, au wafanyakazi wa mawakala wanaoshiriki katika kukusanya, kutunza, au kutumia taarifa) au kutumika kwa ajili ya dhumi lolote zaidi ya kutekeleza huduma za UPATIKANAJI Mapema.

Kuna mambo yasiyofuata kawada, hata hivyo, kwenye hitaji la idhini ya mzazi. Kwa mfano, maafisa wa elimu wanaweza kuweka wazi kumbukumbu za elimu bila ya dihini pale inapohitajika kujibu dharura ya afya au usalama. Kama una maswali kuhusu mambo yasiyofyata kawaida ya FERPA, tafadhali wasiliana na mratibu wako wa huduma.

Jambo moja muhimu la pekee la FERPA linaruhusu mawakala wa elimu kuhamisha kumbukumbu bila idhini ya wazazi kwa mawakala wengine wa elimu ambako mtoto amejiunga au anatarajiwa kuijunga. Kwa sababu hiyo, na kuhakikisha uhamisho usio na tatizo kutoka UPATIKANAJI Mapema kwenda IDEA Sehemu B (Elimu maalumu ya utotonii), kama uhamisho wa mtoto wako kwenda kwenye huduma za elimu ya awali Sehemu B katika umri wa miaka mitatu, idhini yako haitahitajika chini ya FERPA na IDEA. Kumbukumbu za mtoto wako za UPATIKANAJI Mapema zitatumwa kwa Wakala wa Elimu wa Eneo anayehusika na huduma za elimu maalumu katika wilaya ya shule yako.

Punde taarifa itakapokuwa sehemu ya kumbukumbu za mtoto wako za UPATIKANAJI Mapema, zinalindwa na FERPA na zinaweza kutolewa kwa mujibu wa sheria za FERPA. Hii inajumuisha taarifa za kitabibu au tathmini ya nje iliyoruhusiwa kwenye kumbukumbu ya mtoto wako.

### **Iwapo nikikataa kutoa idhini yangu inapohitajika kuweka wazi taarifa za kumbukumbu za mtoto wangu za UPATIKANAJI Mapema, wakala atafanyaje?**

Wakala atakutana nawe na kuelezea namna ambavyo kukataa kwako kutoa idhini kunaweza kuathiri uwezo wa mtoto wako kupokea huduma za UPATIKANAJI Mapema. Wakala wa umma hawezi kutawala kukataa kwako kutoa idhini.

**Kuna hatua zozote zingine ambazo wakala wa umma anazichukua kulinda na kuhifadhi usiri na faragha ya mtoto wangu?**

1. Afisa mmoja katika kila wakala atawajibika kuhakikisha usiri wa taarifa binafsi za utambuzi;
2. Watu wote wanaokusanya au wanaotumia taarifa binafsi za utambuzi lazima wapate mafunzo au maelekezo kuhusu usiri na faragha; na
3. Kila wakala anayeshiriki atahifadhi kwa ajili ya ukaguzi wa umma orodha mpya ya majina ya wafanyakazi na nafasi zao ndani ya wakala ambao wanaweza kupata taarifa binafsi za utambuzi.

**Nini kitatokea kwenye kumbukumbu za mtoto wangu za UPATIKANAJI Mapema pale ambapo hazihitajiki tena?** Wakala wa umma atakujulisha wakati taarifa binafsi za utambuzi zinakusanya, zinatunzwa, au kutumika kwamba hazihitajiki tena ili kutoa huduma za kuingilia kati mapema kwa mtoto wako. Taarifa lazima ziharibiwe ukiomba kama kumbukumbu hazihitajiki tena.

Maamuzi ya kwamba lini kumbukumbu hazihitajiki tena kwa kiasi kikubwa linaegemea katika umakini wa wakala wa umma. Kumbukumbu itatunzwa hadi pale itakapokuwa haihusiani tena na utoaji wa huduma za UPATIKANAJI Mapema na hazihitajiki tena kwa ajili ya madhumuni ya ukaguzi mahesabu na uwajibikaji. kwa kiwango kidogo, kumbukumbu inayohitajika kwa madhumuni ya ukaguzi wa mahesabu na uwajibikaji lazima itunzwe kwa muda wa miaka mitano baada ya shughuli ambayo UPATIKANAJI Mpaema au fedha zingine zimetumika.

**Kuna baadhi ya kumbukumbu ambazo wakala wa UPATIKANAJI Mapema hatakiwi kuziharibu?**

Ndiyo. Wakala anaweza kuweka kumbukumbu za kudumu za ina la mtoto wako, tarehe ya kuzaliwa, taarifa za mawasiliano za mzazi (iliwemo jina na namba ya simu), majina ya waratibu wa huduma na watoaji wa UPATIKANAJI Mapema, na takwimu za kutoka (iliwemo mwaka na umri kabla ya kutoka na program yoyote aliyoingia baada ya kutoka). Taarifa hizi zinaweza kutunzwa bila ukomo wa muda.

**MAELEZO:**

## MIKUTANO

Maamuzi mengi muhimu yanafanya kwa ajili ya mtoto wako kwenye mikutano. Kipengele hiki kinakueleza haki zako za mikutano ni zipi.

### **Wakati gani ambapo mikutano unahitajika au siyo lazima?**

Unahitajika: Sheria za UPATIKANAJI Mapema na sheria ya IDEA Sehemu C zinahitaji mikutano kutengeneza IFSP ya awali kama mtoto wako atabainika kustahili kwaajili ya UPATIKANAJI Mapema, mikutano mkuu kutathmini (na kurekebisha, kwa kuwa ni muhimu) IFSP ya mtoto wako. Sheria pia inahitaji mikutano wakati mtoto wako anabadilishwa kutoka kwenye UPATIKANAJI Mapema.

Si lazima: Sheria inahitaji kwamba IFSP ya mtoto wako inapitiwa mara kwa mara (angalau kila baada ya miezi sita). Kipindi hicho cha mapitio kinaweza kuwa kwenye mikutano, lakini mikutano hauhitajiki. Timu ya IFSP ya mtoto wako pia inaweza kukutana kama itaamua mikutano utamsaidia mtoto wako.

### **Mambo gani yanahitajika kwaajili ya wapi na lini mikutano inafanyika?**

Mikutano kwa ajili ya UPATIKANAJI Mapema lazima ufanyike:

- katika maeneo na katika nyakati ambazo zinatafaa kwako; na
- Katika lugha ya asili ya familia yako au njia nyingine za mawasiliano ambayo unatumia, isipokuwa ijulikane kwamba haiwezekani kufanya hivyo.

Lazima uwe sehemu ya ufanyaji mipango ya mikutano. Wewe na washiriki kwengine wa mikutano lazima mpate walaka wa maandishi juu ya mikutano mapema kabla ya tarehe ya mikutano kuhakikisha kwamba mnaweza kuhudhuria.

### **Nani lazima ahudhurie mikutano wa IFSP?**

Mikutano ya awali ile mikuu, vile vile mikutano ya kutengeneza mpango wa kubadili kwa ajili ya mtoto wako, lazima ijumuushe washiriki wafuatao:

1. **Wewe!** (“Mzazi au wazazi wa mtoto”);
2. Ndugu wengine katika familia, kama ilivyoombwa na mzazi, kama inawezekana kufanya hivyo;
3. Wakili au mtu mwingine nje ya familia, kama mzazi ameomba kwamba mtu huyo ashiriki;
4. Mratibu wa huduma anayewajibika kwa ajili ya utekelezaji wa IFSP;
5. Mtu au watu ambao moja kwa moja wanahusika katika kuendesha tathmini ya mtoto wako na uchunguzi wa mtoto wako na familia yako; na
6. kama inafaa, watu ambao watakuwa wakitoa huduma za UPATIKANAJI Mapema kwa mtoto au familia yako.

Iwapo mtu aliyetajwa kwenye kipengele cha 5 hawezi kuhudhuria, Mdhamsini wa Mkoa atafanya utaratibu kuhakikisha ushiriki wa huyo mtu kuitia njia zingine, ikiwemo moja ya zifuatazo: kushiriki katika mikutano kwa simu, kutumwa mwakilishi mwenye kibali kwenye mikutano, au kufanya kumbukumbu zinazohitajika zipatikane mikutanoni.

## **WAZAZI AU WAZAZI MBADALA**

Wazazi ni wabia muhimu katika huduma za UPATIKANAJI Mapema. Ni muhimu kubainisha yupi ni mzazi wa mtoto mchanga au mtoto anayetembea. Sheria za IDEA na UPATIKANAJI Mapema zinatoa maana ya “mzazi.”

### **Mzazi ni nani?**

“Mzazi” inamaana:

1. Mzazi wa mtoto wa kibaolojia au wa kuasili;
2. Mzazi mlezi, isipokuwa sheria ya nchi, taratibu, au majukumu ya kimkataba na kitengo cha nchi au cha ndani kinazuia mzazi mlezi kuwa kama mzazi;
3. Mlezi kwa ujumla ana mamlaka ya kuwa kama mzazi wa mtoto, ana mamlaka ya kufanya maamuzi ya kuingilia kati mapema, elimu au maamuzi ya kimaendeleo kwa ajili ya mtoto (lakini siyo jiji kama mtoto ni ni kata ya hilo jiji);
4. Ukaimu binafsi katika nafasi ya mama mzazi au wa kuasili( ikiwemo bibi na babu, mzazi wa kufiki, au ndugu wengine) ambaye anaishi na mtoto,au mtu binafsi ambaue kisheria anawajibika kwa ustawi wa mtoto; au
5. Mzazi mbadala ambaye amechaguliwa kwa mujibu wa sheria za shirikisho na sheria za UPATIKANAJI Mapema.

### **Nini kitatokea iwapo mtu zaidi ya mmoja wanakidhi maana ya mzazi?**

Sheria zifuatazo zitatumika kubaini iwapo pande inastahili kuwa kama “mzazi.”

1. Isipokuwa kama ilivyotolewa kwenye kipengele kijcho, mzazi wa kibaolojia au wa kusili, anapajaribu kuwa kama mzazi chini ya sura hii na pale ambapo zaidi ya pande moja ina sifa za kuwa mzazi, lazima akubaliwe kuwa mzazi isipokuwa pale ambapo mzazi wa kibaolojia au wa kuasili hana mamlaka kisheria ya kufanya maamuzi ya kielimu au huduma za kukuilingilia kati mapema kwa ajili ya mtoto.
2. Iwapo hukumu au amri ya kimahakama inabainisha mtu mahususi au watu kuwa kama “mzazi” wa mtoto au kufanya maamuzi ya kielimu au huduma za kukuilingilia kati mepema kwa niaba ya mtoto (isipokuwa kama mzazi mbadala), basi mtu au watu hao lazima tambuliwe kama “mzazi” kwa dhimuni la Sehemu C ya Sheria, isipokuwa kwamba kama mtoaji wa EIS au wakala wa umma anatoa huduma zozote kwa mtoto au kwa mwanafamilia yeyote wa mtoto huyo, mtoaji huyo wa EIS au wakala wa umma hawezি kuwa kama mzazi kwa mtoto huyo.

### **Kwanini mzazi mbadala?**

Wadhamini wa Mkoa wanahitaji kubaini kwamba kila mtoto ana mzazi wa kushiriki kwenye taratibu za UPATIKANAJI Mapema. Iwapo yoyote kati ya hali zifuatazo ipo, Mdhhamini wa Mkoa atabaini iwapo mzazi mbadala ni muhimu kwa ajili ya mtoto:

1. Hakuna mzazi anayeweza kubainishwa;
2. Kwa juhudhi za kina, hakuna mzazi anayeweza kupatikana ; au
3. Mtoto ni kata ya Jiji na jaji anaendesha kesi ya mtoto; au badala yake anachaguliwa mzazi mlezi.

Ni wajibu wa Mdhhamini wa Mkoa kubainisha mtoto yupi anahitaji kaimu mzazila na kumpa mtu kazi ya kuwa mbadala wa mzazi wa mtoto.

### **Sifa za Mzazi Mbadala ni zipi?**

Mzazi mbadala lazima:

1. Asiwe na mslahi yake binasi au kitaalamu ambayo yanakinzana na maslahi ya mtoto;
2. Ana maarifa na ujuzi ambao unahakikisha uwakilishi sahihi wa mtoto; na
3. Asiwe mwajiriwa wa Idara ya Elimu ya Iowa, Mdhamsini wa Mkoa, au wakala mwingine yeote ambaye anahusika kwenye elimu utunzaji wa mtoto.

Mtu ambaye pengine anasifa za kuwa mzazii mlezi hachukuliwi kama mfanyakazi wa wakala tu kwasababu analipwa na wakala kufanyakazi kama mzazi mlezi.

### **Nani anamteua mzazi mbadala?**

Mdhamsini wa Mkoa anaweza kumteua mzazi mbadala katika namna yeote ambayo sheria inaruhusu. Kwa kwa upande mwingine, mahakama inaweza kuchukua kesi mtoto ambaye ni “kata ya jiji” (katika uangalizi, kwenye uangalizi wa wakala wa ustawi wa mtoto wa umma) inaweza kuteua mzazi mlezi kwa ajili ya mtoto. Mzazi mlezi aliyeteuliwa na mahakama lazima atomize sifa tatu zilizotajwa hapo juu.

### **Majukumu ya mzazi mbadala ni yapi?**

Mzazi mbadala anaweza kumwakilisha mtoto katika masuala yote yanayohusiana na tathmini na uchunguzi wa mtoto, maendeleo na utekelezaji wa IFSP (ikiwemo mapitio ya mwisho ya tathmini), utolewaji wa huduma za kuingilia kati mapema zinazoedelea, na haki zingine zozote chini ya UPATIKANAJI Mapema na IDEA.

### **MAELEZO:**

## **CHAGUZI ZA UTATUZI WA MIGOGORO**

Kuna chaguzi tatu katika sheria ya UPATIKANAJI Mapema na Sehemu C ya IDEA kwa ajili ya kutatua migogoro. Chaguzi hizo ni:

- upatanisho,
- malalamiko ya Jimbo, na
- Malalamiko ya taratibu za malipo.

Chaguzi hizo zitaelezewa kwenye kipengele kijacho cha mwongozo huu.

Kwa kuongeza katika hizo chaguzi tatu, kila Mdhagini wa Mkoa ana utaratibu unaoitwa Uwezeshaji Utatuzi ambao unaweza kutumika. Uwezeshaji Utatuzi ni njia ya kutatua tofauti, badala ya, au kabla ya kutumia taratibu rasmi zilizoelezewa kwenye mwongozo huu. Mwezeshaji utatuzi husaidia kutatua tofauti juu ya huduma za UPATIKANAJI Mapema na masuala kati ya wazizi, wakala wa uma, na watoaji wa sekta binafsi.

Kama tofauti zinatokea, majadiliano ya wazi ni hatua ya kwanza muhimu katika kutatua hizo tofauti. Mtu wa tatu anaweza kutoa dhumuni la kupitia hoja zao pande zote katika kusaidia hitimisho lenye mafanikio. Mwezeshaji wa Utatuzi ni mpatanishi aliyepatiwa mafunzo na ni upande wa tatu usiofungamana na upande wowote. Mwezeshaji wa Utatuzi anaweza kutofungamana na upande wowote kutoka kwenye mkoa wako wa UPATIKANAJI Mapema au, kama ni muhimu, mtu fulani kutoka mkoa mwingine au aliyetolewa na Idara ya Elimu. H u d u m a y a Mwezeshaji Utatuzi e Resolution Facilitator inatolewa bila gharama kwa watoa huduma kwako au mtoto wako.

Kama ni muhimu kutumia utaratibu wa Mwezeshaji wa Utatuzi kabla ya kutumia njia rasmi tatu zilizoelezewa kwenye mwongozo huu.

### **MAELEZO:**

## **UPATANISHO**

Idara ya Elimu Iowa na Mwadhamini wa Mkoa wanatunza taratibu kuziwezesha pande kutatua migogoro kuitia mapatano. Upatanisho ni hiari kwa upande wa pande zote na unafanywa na mpatanishi mwenye sifa na asiyé na upendeleo ambaye amepatiwa mafunzo juu ya mbinu za upatanisho mzuri. Upatanisho unaweza kutokea wakati wowote, hata kabla ya kufungua malalamiko ya taratibu za malipo. Upatanisho hautumiki kuchelewsha au kukataa haki yako ya kufungua malalamiko ya taratibu za malipo, hali zozote zingine chini ya UPATIKANAJI Mapema.

Fomu ya kuomba upatanisho iko kwenye ukurasa wa 20 wa mwongozo huu.

### **Wapi naweza kuwapata watu ambao ni wapatanishi na nani anawalipa kwa ajili ya upatanisho?**

Idara ya Elimu ya Iowa:

1. Inatunza orodha ya watu ambao wpatanishi wenyé sifa na ufahamu juu ya sheria na taratibu zinazohusiana na utoaji wa huduma za UPATIKANAJI Mapema;
2. Huchagua wapatanishi bila mpango maalumu, kwa kuzunguuka, au mfumo mwingine usio na upendeleo; na
3. Hulipa gharama za utaratibu wa upatanisho, ikiwemo gharama za mikutano kuhamasisha upatanisho pale ambapo upande umechagua kutokutumia upatanisho.

### **Nitajuaje kwamba mpatanishi hana upendeleo?**

Mtu anayefanya kazi kama mpatanishi:

- Hawezi kuwa mwajiriwa wa Idara ya Elimu Iowa au wakala wa umma au mtoe huduma wa kujitegemea ambaye anatoa huduma moja kwa moja kwa mtoto wako; na
- Lazima awe hana mgogoro wa kimaslahi binafsi st au kitaalamu;

Mtu ambaye pengine ana sifa siyo mwajiriwa wa Idara ya Elimu Iowa kwasababu analipwa kuwa mpatanishi.

### **Mambo gani nahitaji kuyafahamu kuhusu hatua za upatanisho?**

1. Kila mkutano katika hatua za upatanisho lazima upangwe kwa kuzingatia muda na lazima ufanyike mahali ambapo panafaa kwa pande zote zenye mgogoro.
2. Iwapo wewe na wakala wa umma mnatatua mgogoro kwa njia ya upatanisho, wewe na wakala wa umma lazima mtekeleze makubaliano yanayohitajika.
3. Wote wewe na mwakilishi wa wakala wa umma ambaye ana mamlaka ya kuijunga mawakala hao lazima wasaini makubaliano yanayohitajika kisheria.
4. Makubaliano ya upatanisho yaliyo kwenye maandishi na kusainiwa yantumika katika Mahakama za Jiji zenye uwezo au mahakama ya wilaya ya Marekani
5. Majadiliano ambayo yanatokea wakati wa upatanisho ni siri na hayawezi kutumika kama ushahidi kwenye kesi ya utaratibu wa malipo au kesi za madai za mahakama yoyote ya shirikisho au jimbo.

### **Inakuwaje kama sitaki kutumia utaratibu wa upatanisho?**

Mdhamini wa Mkoa anaweza kuwapa wale wasiotumia utaratibu wa upatanisho fursa ya kukutana na upande usiopendela katika muda na mahalali panapowafaa wazazi.

**Upande usiopendelea ni upi?**

1. Kitengo kingine cha upatanisho kinachofaa;
2. Kituo cha Mafunzo na Taarifa cha Wazazi Iowa (katika Iowa, hii ni Kituo cha Rasilimali za Upatikanaji kwa Watoto Maalumu (ASK); au
3. Kituo cha Rasilimali cha Jamii.

**Upande usiopendelea ungefanya nini?**

Upande usiopendelea ungeelezea faida na kuhamasisha matumizi ya utaratibu wa upatanisho kwako.

**Wakati ombi langu la upatanisho linasubiri kushughulikiwa, huduma gani mwanangu anapokea?**

Wakati ombi lolote la upatanisho linasubiri kushughulikiwa na na kwa siku kumi baada ya mukutano huo wa upatanisho ambao hakuna makubaliano yaliyofikiwa, isipokuwa wakala na wazazi wa mtoto wakubaliane vinginevyo, mtoto anayehusika kwenye mukutano wowote wa upatanisho lazima aendelee kupata huduma sahihi za kuingilia kati mapema zilizobainishwa kwenye IFSP katika mahali ambapo panafaa kwa wazazi.

Iwapo upatanisho unahusisha maombi ya huduma za awali chini ya UPATIKANAJI Mapema, mtoto lazima apate huduma zile ambazo hazipo kwenye mgogoro.

**MAELEZO:**

## **MALALAMIKO YA JIMBO YA IDEA**

Sheria inahitaji Idara ya Elimu Iowa kuwa na utaratibu wa kuchunguza malalamiko ambayo wakala amevunja Sehemu C ya IDEA au Sheria za UPATIKANAJI Mapema Iowa. Nakala ya fomu ya kufungua malalamiko ya jimbo iko kwenye ukurasa wa 22 wa mwongozo huu.

### **Idara ya Elimu Iowa inatoa taratibu za kufungua malalamiko ya jimbo chini ya UPATIKANAJI Mapema?**

Idara ya Elimu inataratibu za kimaandishi kwa ajili ya:

1. Utatuzi wa malalamiko yoyote, ikiwemo malalamiko yaliyofunguliwa na shirika au mtu binafsi kutoka Jimbo lingine, kwa kuitoa kwa ajili ya kufungulia malalamiko na Idara ya Elimu Iowa, na
2. Kusambaza kwa upana taratibu za jimbo kwa wazazi na pande zenyet maslahi, ikiwemo vituo vya mafunzo na taarifa vya wazazi, mawakala wa ulinzi na ushawishi, vituo vya kuishi vya kujitegemea, na vyombo vingine husika.

### **Idara ya Elimu Iowa itafanyaje kama itagundua kushindwa kutoa huduma sahihi za UPATIKANAJI Mapema?**

Katika kutatua malalamiko ambayo Idara ya Elimu Iowa imegundua kushindwa kutoa huduma sahihi, Jimbo lazima lishughulikie:

1. Kushindwa kutoa huduma sahihi, ikiwemo hatua za sahihi za kushughulikia mahitaji ya mtoto, na
2. Upatikanaji wa baadaye wa huduma kwa watoto wote wenye ulemavu.

### **Taratibu za Malalamiko ya jimbo ya Idara ya Elimu inajumuisha mambo gani?**

Kwenye taratibu zake za malalamiko, Idara ya Elimu Iowa inajumuisha ukomo wa muda wa siku 60 za kalenda baada ya kufunguliwa kwa malalamiko:

1. Kushughulikia uchunguzi wa kujitegemea wa mahali, iwapo Idara ya Elimu Iowa itabaini kwamba uchunguzi ni wa lazima;
2. Kumpa mlalamikaji fursa ya kuwasilisha taarifa za ziada, aidha kwa mdomo au maandishi, kuhusu mashtaka yaliyomo kwenye malalamiko;
3. Kumpa wakala wa umma fursa ya kujibu malalamiko, ikiwemo, kwa kiasi kidogo:
  - a. Katika uangalifu wa wakala wa umma, pendekezo la kutatua malalamiko na
  - b. Kwa idhini ya wazazi, fursa kwa ajili ya wakala kuhusisha wazazi katika upatanisho, au njia nyingine mbadala ya kutatua mgogoro;
4. Kupitia taarifa zote zinazohusiana na kufanya utambuzi unaojitegemea kama iwapo wakala wa umma anavunja mahitaji ya IDEA; na
5. Kutoa maamuzi kwa maandishi kwa mlalamikaji ambayo yanashughulikia kila shitaka kwenye malalamiko na yanabeba:
  - a. Matokeo ya ushahidi na hitimisho, na
  - b. Sababu za maamuzi ya mwisho ya Idara ya Elimu Iowa.

### **Muda wa zaidi ya siku 60 unaruhusiwa?**

Taratibu za Idara ya Elimu zinaruhusu kuongezeka kwa muda wa ukomo kama tu:

1. Kuna hali isiyo ya kawaida inayohusiana na lalamiko husika, au
2. Wazazi na wakala wa umma wamekubali kuongeza muda kufanya kazi hiyo.

### **Maamuzi ya lalamiko yanatekelezwaje?**

Taratibu za Idara ya Elimu zinajumuisha hatua za utekelezaji wa maamuzi yake ya mwisho, kama inahitajika, kujumuisha:

1. Shughuli za msaada wa kiufundi;
2. Majadiliano; na
3. Hatua za jumla za kufikia makubaliano.

### **Nani anaweza kufungua malalamiko na inafanyikaje?**

Shirika au mtu binafsi anaweza kufungua malalamiko ya maandishi yaliyosainiwa lazima yajumuise maelezo kwamba wakala wa umma amevunja mahitaji ya Sehemu C ya IDEA. Malalamiko lazima yajumuise:

1. Ushahidi unaohusiana na maelelzo;
2. Sahihi na taarifa za mawasiliano ya mlalamikaji; na
3. Mlalamikaji lazima adai kwamba uvunjwaji umetokea siyo zaidi ya mwaka mmoja kabla ya tarehe ambayo malalamiko yalipokelewa.

